

## Kujifunza Biblia katika Makundi Madogo

**Utangulizi:** Kujifunza Biblia kwa Ugunduzi kumejengwa katika kanuni zifuatazo:

1. Biblia ni Neno la Mungu, lililovuviwa na Roho Mtakatifu, kuongoza, kutia moyo, kuonya, kujenga Imani, na kufundisha.
2. Mungu amejidhihirisha katika Maandiko – kupitia mamia ya visa, nyimbo, mithali, na unabii. Ili kumfahamu Mungu vema zaidi, tunahitaji kwenda katika chanzo: Neno lake lililovuviwa.
3. Roho Mtakatifu yule yule aliyevuvia Biblia anaweza kutuongoza kujifunza. Tunachopaswa kufanya ni kuomba.
4. Biblia ndiyo kitu cha pekee tunachohitaji ili kujenga Imani na maisha yetu.
5. Kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, mtu ye yote anaweza kuielewa Biblia. (Msomi au asiye msomi, watu wazima au watoto, wanaume au wanawake).
6. Kujifunza Biblia ndiyo namna “tunavyokula” chakula cha kiroho ili kuwa imara.
7. Kila muumini hujifunza namna ya “kula” peke yake, na si kulishwa (kula chakula ambacho kimekwisha meng’enywa).
8. Kwa Kujifunza Biblia kwa Ugunduzi, Biblia inaweza kujifunzwa na Mtu binafsi au katika makundi.
9. Watoto, wasiojua kusoma, au vipofu wanapokuwa sehemu ya kundi la Kujifunza Biblia kwa Ugunduzi, hujifunza pia Neno la Mungu moja kwa moja. Hakuna anayeachwa nje.
10. Kadri tunavyojifunza katika makundi, tunajifunza kutoka kwa kila mmoja wetu. Kila mmoja hushiriki.
11. Kujifunza Biblia kwa Ugunduzi ni njia rahisi ambayo watu wanaweza kujifunza Biblia peke yao kwa uongozi wa Roho Mtakatifu.

### **Hatua katika Kuongoza Kundi la Kujifunza Biblia kwa Ugunduzi**

- Kuwe na kikundi na muda wa kukutana, eneo na mazingira viwe vimepangwa vizuri.
- Siku ya kwanza waeleze watu, hatua zifuatazo ambazo mtazitumia katika kujifunza Biblia.
  1. Ruhusu mtu mmoja kuomba ombi fupi kwa ajili ya Roho Mtakatifu kuwa mwalimu na kiongozi.
  2. Soma pamoja kifungu (Kwa wale wanaoweza kusoma, pokezaneni kusoma ili kumhusisha kila mmoja. Kwa kundi la wasiojua kusoma, eleza au soma hadithi kwa ajili ya kundi hilo kama ilivyo ktk Biblia).
  3. Pitia taarifa muhimu pamoja ili kuhakikisha kila mmoja anazikumbuka zote – “Nini kilitokea mwanzo? Nini kilifuata? n.k. Watu katika hadithi hiyo walikuwa ni akina nani?” n.k.
  4. Soma tena (au eleza tena) kifungu hicho. Waombe watu kutafakari unapoirudia hadithi hiyo.
  5. Muulize kila mtu kile “alichoona” katika hadithi hiyo.
  6. Mwombe mtu aombe tena kwa ajili ya Roho Mtakatifu kuongoza uelewa wetu. Ombi fupi sana.
  7. Uliza na jadili maswali yafuatayo (Kumbuka lengo ni kumhusisha kila mmoja, tukikumbuka kwamba Roho Mtakatifu hunena na wote, na si mtu mmoja au wawili tu<sup>i</sup>):
    - Je, hili hutueleza nini kumhusu Mungu?
    - Je, hili hutueleza nini kuhusu watu (nikiwemo) na chaguzi tunazofanya?
    - Ni nini kipo katika hili ambacho ninapaswa kufuata au kutii? Kinawezaje kuathiri maisha yangu?
  8. Je, unamfahamu mtu ambaye unaweza kushirikiana nae hili?
  9. Funga kwa kuomba pamoja. Lenga katika:
    - a. Maamuzi ya vitu vya kufuata/kutii
    - b. Ugunduzi mpya uliopatikana kumhusu Mungu na maisha.

---

<sup>i</sup> **Tahadhari:** Kutafuta mtu wa kushirikiana nae hadithi hiyo ikiwa una kundi zaidi ya moja, ruhusu makundi hayo tofauti kushiriki utambuzi wao. Usiwe mtu wa kutoa kila jibu, acha wafanye ugunduzi taratibu. Roho Mtakatifu hutufundisha na kutuongoza sote na tunajifunza kutoka kwa kila mmoja wetu. Waongoze watu kuyajibu hayo maswali wenyewe na usiruhusu mtu mmoja hasa kiongozi kujibu maswali yote. Waongoze watu kusema kile Roho wa Mungu alichowaonyesha kwa namna rahisi. Majibu yatokane na Biblia katika kipengele mlicojifunza siku hiyo tu. Somo lisiwe refu sana.

*Mwongozo huu, umetoka katika Kitengo cha Global Mission GC 2019 | Zipo Sababu muhimu za Kibiblia za kwa nini maelekezo yametolewa kama yalivyo. Kwa semina kamili na maelezo haya tembelea:*

<https://netc.adventistafrica.org/huduma> kisha nenda chini kabisa kwenye kipengele cha “**Miongozo mbalimbali.**”